TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Imezuiliwa hadi
Jumatatu, Oktoba 11, 2010
8:30 GMT

Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana na:
Michael Rubinstein, m.rubinstein@cgiar.org, +1 (202) 862-5670
Simone Pott, Simone.Pott@welthungerhilfe.de, +49 228-2288-132
Paul O'Mahony, Paul.OMahony@concern.net, +353 (1) 479 1309

Imarisha Lishe Bora Ili Kupunguza Njaa Ulimwenguni, Ripoti Mpya ya Kipimo cha Kiwango cha Njaa Duniani (Global Hunger Index), Inaonyesha.

Washington, D.C. – Utapiamlo au ukosefu wa lishe bora kati ya watoto wa chini ya miaka miwili ni moja wapo ya changamoto kubwa katika kupunguza njaa ulimwenguni na huweza kuathiri vibaya afya, uzalishaji, na hali ya kustawi kimapato. Hii ni kulingana na Kipimo cha Kiwango cha Njaa Duniani cha 2010.

Ripoti iliyotolewa kabla ya Siku ya Chakula Duniani (Oktoba 16) kwa mwaka wa tano sasa, imechapishwa na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Sera ya Chakula, - *International Food Policy Research Institute (IFPRI)*- na mashirika yasiyo ya kiserikali, *'Welthungerhilfe'* na *'Concern Worldwide'*.

Kipimo cha Kiwango cha Njaa Duniani , hupima nchi kulingana na viashiria vitatu vilivyotoshana kiuzani: kiwango cha watu wasio na lishe bora, kiwango cha watoto chini ya umri wa miaka mitano, walio na uzito wa chini ya inavyostahili; na kiwango cha vifo vya watoto wadogo. Sababu kuu ya kutofikia malengo ya lishe bora ulimwenguni ni utapiamlo kwa watoto, ambao huchangia kiwango takriban nusu ya matokeo.

“Kuboresha matokeo yao, nchi nyingi lazima ziimarishe mbinu za kupunguza utapiamlo katika watoto. Utafiti unaonyesha kuwa, nafasi bora ya kuimarisha viwango vya lishe huanzia wakati mimba inapotungwa hadi umri wa miaka miwili. Ikiwa mtoto hakupata lishe bora kabla ya miaka miwili, hupata athari mbaya baadaye zisizoweza kurekebishika”. Maneno haya ni usemi wa Marie Ruel, mkurugenzi wa IFPRI, kitengo cha umasikini, afya na lishe bora na mwandishi mwenza wa ripoti hii.

Kipimo cha kiwango cha njaa kilipatikana baada ya utafiti uliofanywa katika nchi 122 zinazoendelea. Utafiti unaonyesha kwamba nchi ishirini na tisa kati ya hizo zina viwango vya kutisha mno vya njaa. Nyingi kati yake ni nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara na Asia Kusini.

Licha ya kuwa viwango vya juu vya ukosefu wa chakula (njaa) huwa katika nchi hizi, Asia Kusini imepiga hatua mbele tangu mwaka wa 1990.

Katika Asia Kusini, viwango vya chini vya lishe bora, elimu na hadhi ya wanawake, ni baadhi ya mambo makuu yanayochangia utapiamlo kwa watoto chini ya miaka mitano.

Katika Kusini mwa Jangwa la Sahara, utepetevu wa serikali, mizozo, migogoro ya kisiasa na viwango vya juu vya ukimwi ni baadhi ya mambo yanayochangia vifo vya watoto na kiwango kikubwa cha watu ambao hawatimizi viwango vyao vya kalori. Katika baadhi ya nchi kama vile Burundi, Madagascar na Malawi takriban nusu ya watoto wamedumaa kwa sababu ya lishe duni.

Tatizo hili linaweza kupunguzwa kwa asilimia 25 – 36 kwa kutoa huduma za kiafya na mipango ya lishe bora kwa watoto chini ya miaka miwili na mama zao, wakati wa mimba na wakati wa kunyonyesha.

“Afya ya wanawake, hasa ya akina mama, ni muhimu katika kupunguza utapiamlo kwa watoto. Akina mama ambao hawakupata lishe bora utotoni, aghlabu huzaa watoto wenye uzani wa chini na hivyo basi kuendeleza mzunguko wa utapiamlo,” asema Bärbel Dieckmann, mwenyekiti wa Welthungerhilfe. "Mipango ya lishe bora inafaa ilengwe kwa wasichana na

wanawake katika mzunguko wa maisha yao, hasa wanapovunja ungo na kabla ya kuwa wajawazito:".

Ripoti inapendekeza kuwa ili kupunguza njaa duniani, mataifa lazima:

- yalenge mikakati ya kunufaisha zaidi wanawake wajawazito, wanaonyonyesha na watoto, kwa miaka miwili ya kwanza ya maisha yao.
- yaangazie visababishi vya utapiamlo vikiwemo umasikini, upendeleo wa kijinsia na mizozo.
- yashirikishe, yahamasishe na kuwafadhili wafanyikazi nyanjani ili kuboresha lishe; na
- yapatie lishe bora haswa kwa watoto wadogo, kipaumbele kisiasa.

Mkurugenzi mtendaji wa Concern Worldwide, Tom Anorld alisema, " Ni muhimu mno kuhakikisha lishe bora katika siku 1,000 za kwanza. Ripoti hii ya Kipimo cha Kiwango cha Njaa Duniani (The Global Hunger Index) inaonyesha mapendekezo ya wazi, ili kujulisha na kuhamasisha jamii ya kimataifa kuchukua hatua mwafaka juu ya hili Suala.

###

Kipimo cha Kiwango cha Njaa, kurasa zenye takwimu , na makala yanayohusiana, yanapatika kwa: http://www.ifpri.org/pressroom/briefing/2010-global-hunger-index-crisis-child-undernutrition

Taasisi ya kimataifa ya utafiti wa sera ya chakula- International Food Policy Research Institute (IFPRI)- hutafuta mbinu endelevu za kumaliza njaa na umaskini. IFPRI, ni moja wapo ya vituo15 vinavyofadhiliwa na kundi la Consultative Group on International Agricultural Research, ambalo ni muungano wa serikali 64,mashirika ya kibinafsi na mashirika ya kimataifa na ya kikanda. Tafadhali tembelea tovuti yetu kupitia www.ifpri.org.

Welthungerhilfe, ni moja wapo ya mashirika makuu ya msaada yasiyo yakiserikali huko ujerumani. Hutoa msaada wa jumla kutoka mahali pamoja, kuanzia msaada wa dharura hadi kwa mipango ya ukarabati na vile vile miradi ya muda mrefu kupitia ushirikiano na mashirika ya nchi husika,kwa kutumia kanuni ya 'saidia kwa lengo la kujisimamia'. Tangu shirika hili lilipoanzishwa mwaka wa 1962, zaidi ya miradi 6,247 imefanywa katika nchi 70. Miradi hii ilifadhiliwa na msaada wa jumla ya bilioni €2.03, kwa malengo ya kuwa na ulimwengu usio na njaa wala umasikini. Kwa taarifa zaidi tafadhali tembelea www.welthungerhilfe.de.

Concern Worldwide ni shirika la kimataifa la kibinadamu lisilo la kiserikali ambalo limejitolea kupunguza mateso na malengo yake ni kumaliza kabisa umasikini uliokithiri, katika nchi masikini zaidi duniani. Umma unaweza kupokea taarifa za mara kwa mara kwenye mtandao kupitia tovuti ya Concern, www.concern.net.